

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BARAZA LA MITIHANI  
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**614**

**MAARIFA YA JAMII**

**Muda: Saa 3**

**Alhamisi, 9 Mei 2013 asubuhi**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A na maswali **mawili (2)** kutoka katika kila sehemu B na C.
3. Zingatia maelekezo ya kila sehemu na ya kila swali.
4. Andika majibu yako kwa kalamu ya wino wa bluu au mweusi isipokuwa **Michoro** ambayo itachorwa kwa penseli.
5. Vikokotozi na simu za mkononi **haziruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
6. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha **kujibia**.

Ukurasa wa 1 kati ya 3



## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. (a) Eleza maana ya kipimo cha ramani.  
(b) Bainisha aina kuu za ramani.  
(c) Bainisha njia zinazotumika kuwasilisha kipimo cha ramani.
2. (a) Eleza kwa kifupi dhana ya Kanda za Masaa.  
(b) Kama katika mji wa Freetown 15° Magharibi ni saa 11:00 alifajiri, kokotoa muda wa sehemu zifuatazo:  
(i) Morogoro 45° Mashariki                      (ii) Colorado 120° Magharibi
3. (a) Bainisha mizunguko ya Dunia kisha fafaua athari za kila mzunguko.  
(b) Bainisha matokeo yanayoweza kutokana na mzunguko wa mwezi kuizunguka Dunia.
4. Tumia michoro ya mistari ya kontua kuonesha maumbile yafuatayo:  
(a) Pitio                      (b) Genge                      (c) Kigongo                      (d) Uwanda wa juu
5. Eleza tofauti kati ya **Zinjathropus** na **Homohabilis** kama hatua muhimu katika mabadiliko ya kimaumbile ya binadamu wa kale.
6. Bainisha mambo manne yaliyokuwa chanzo cha migogoro ya kisiasa katika nchi za Kiafrika baada ya uhuru.
7. Eleza kwa kifupi sababu nne zilizofanya watawala wa jadi katika Bara la Afrika kushindwa katika jitihada zao za kupinga uvamizi wa wakoloni kutoka bara la Ulaya mwishoni mwa karne ya 19.
8. Kwa kutoa mifano miwili, eleza namna kila aina ya milima ifuatayo inavyotokea:  
(a) Milima mikunjo                      (b) Milima ya tofali                      (c) Milima ya volkano.
9. (a) Eleza kwa kifupi dhana ya ukoloni.  
(b) Toa mifano miwili ya nchi zilizotawaliwa na Uingereza, Ujerumani, Ureno, Ubelgiji na Ufaransa katika nusu ya pili ya karne ya 19.
10. Bainisha sababu nne zilizowafanya wafanyabiashara wa karne ya 19 kutoka Ulaya wajulikane kama vitangulizi vya ukoloni.

## **SEHEMU B (Alama 30)**

Jibu swali **moja (1)** kutoka katika kila kipengele.

### **Kipengele I: Jiografia**

11. Kwa kutumia mifano ya aina ya tabia nchi zilizopo katika ukanda wa Afrika mashariki, eleza uhusiano uliopo kati ya tabia nchi na uoto wa asili.
12. Bainisha hatua zinazoweza kuchukuliwa katika juhudi za kupunguza athari zinazotokana na matetemeko ya ardhi, mafuriko, maporomoko ya ardhi, mmomonyoko wa udongo na ukame.

### **Kipengele II: Historia**

13. Chambua mambo matano yaliyotokea katika mataifa ya nje ambayo yaliongeza kasi katika harakati za kudai uhuru barani Afrika katika nusu ya kwanza ya karne ya ishirini.
14. Chambua athari hasi nne zilizotokana na kugawanywa kwa Bara la Afrika miongoni mwa mataifa ya kibeberu kutoka bara la Ulaya.

## **SEHEMU C (Alama 30)**

Jibu swali **moja (1)** kutoka katika kila kipengele.

### **Kipengele I: Jiografia**

15. Kutokuwepo kwa nidhamu miongoni mwa wanafunzi katika darasa la Jiografia kunatokana na utukutu wa wanafunzi wenyewe. Jadili.
16. Fafanua mambo matano ambayo mwalimu anatakiwa kuzingatia wakati wa kutumia kazimradi kama njia ya kufundishia na kujifunzia somo la Jiografia.

### **Kipengele II: Historia**

17. Mwalimu mwenye uzoefu katika ufundishaji wa somo la Historia hahitaji kuwa na kitabu cha kiongozi cha mwalimu. Jadili.
18. Chambua faida tano za matumizi ya shajara katika kufundisha na kujifunza somo la Historia.